Wimbo Ulio Bora

1 Wimbo ulio bora wa Sulemani.
*Mpendwa**
2 Unibusu kwa busu la kinywa chako,
kwa maana upendo wako unafurahisha kuliko divai.
3 Manukato yako yananukia vizuri,
jina lako ni kama manukato yaliyomiminwa.
Ndiyo sababu wanawali wanakupenda!
4 Nichukue twende nawe, na tufanye haraka!
Mfalme na anilete ndani ya vyumba vyake.
Rafiki
Tunakushangilia na kukufurahia,
tutasifu upendo wako kuliko divai.
Mpendwa
Tazama jinsi ilivyo bora wakupende!
5 Mimi ni mweusi, lakini napendeza,
enyi binti za Yerusalemu,
mweusi kama mahema ya Kedari,
kama mapazia ya hema la Sulemani.
6 Usinikazie macho kwa sababu mimi ni mweusi,
kwa sababu nimefanywa mweusi na jua.
Wana wa mama yangu walinikasirikia
na kunifanya niwe mtunza mashamba ya mizabibu.

---

* **1:1** Kulingana na matumizi ya lugha ya Kiebrania, mnenaji wa kiume na wa kike wametofautishwa kwa kichwa cha Mpenzi na Mpendwa. Wanenaji wengine wamepewa kichwa cha Rafiki. Wakati mwingine haijulikani kwa hakika nani ananena, lakini mapokeo yamefuatwa kutambulisha wanenaji.

Shamba langu mwenyewe la mizabibu nimeliacha.
7 Niambie, wewe ninayekupenda,
unalisha wapi kundi lako la kondoo
na ni wapi unapowapumzisha kondoo wako adhuhuri.
Kwa nini niwe kama mwanamke aliyefunikwa shela
karibu na makundi ya rafiki zako?

Rafiki

8 Kama hujui, ewe mwanamke mzuri kuliko wote,
fuata nyayo za kondoo,
na kulisha wana-mbuzi wako
karibu na mahema ya wachungaji.

Mpenzi

9 Mpendwa wangu, ninakufananisha na farasi jike
aliyefungwa katika mojawapo ya magari ya vita ya Farao.
10 Mashavu yako yanapendeza yakiwa na vipuli,
shingo yako ikiwa na mikufu ya vito.
11 Tutakufanyia vipuli vya dhahabu,
vyenye kupambwa kwa fedha.

Mpendwa

12 Mfalme alipokuwa mezani pake,
manukato yangu yalisambaza harufu yake nzuri.
13 Mpenzi wangu kwangu mimi ni kifuko cha manemane
kati ya matiti yangu.
14 Mpenzi wangu kwangu mimi ni kama kishada cha maua ya mhina

kutoka mashamba ya mizabibu ya En-Gedi.
Mpenzi
15 Tazama jinsi ulivyo mzuri, mpendwa wangu!
Tazama jinsi ulivyo mzuri!
Macho yako ni kama ya hua.
Mpendwa
16 Tazama jinsi ulivyo mzuri, mpenzi wangu!
Ee, tazama jinsi unavyopendeza!
Na kitanda chetu ni cha majani mazuri.
Mpenzi
17 Nguzo za nyumba yetu ni mierezi,
na mapao yetu ni miberoshi.

2

Mpendwa
1 Mimi ni ua la Sharoni,
yungiyungi ya bondeni.
Mpenzi
2 Kama yungiyungi kati ya miiba,
ndivyo alivyo mpendwa wangu kati ya wanawali.
Mpendwa
3 Kama mti wa mtofaa miongoni mwa miti ya msituni,
ndivyo alivyo mpenzi wangu
miongoni mwa wanaume vijana.
Ninafurahia kuketi kivulini mwa mwanaume huyu,
na tunda lake ni tamu kwangu.
4 Amenichukua hadi ukumbi wa karamu,
na bendera ya huyu mwanaume
juu yangu ni upendo.
5 Nitie nguvu kwa zabibu kavu,

niburudishe kwa matofaa,
kwa maana ninazimia kwa mapenzi.
6 Mkono wake wa kushoto uko chini ya kichwa changu,
na mkono wake wa kuume unanikumbatia.
7 Binti za Yerusalemu, ninawaagiza
kwa paa na kwa ayala wa shambani:
Msichochee wala kuamsha mapenzi
hata yatakapotaka yenyewe.

8 Sikiliza! Mpenzi wangu!
Tazama! Huyu hapa anakuja,
akirukaruka juu milimani
akizunguka juu ya vilima.
9 Mpenzi wangu ni kama paa au ayala mchanga.
Tazama! Anasimama nyuma ya ukuta wetu,
akitazama kupitia madirishani,
akichungulia kimiani.
10 Mpenzi wangu alizungumza na kuniambia,
"Inuka, mpendwa wangu,
mrembo wangu, tufuatane.
11 Tazama! Wakati wa masika umepita,
mvua imekwisha na ikapita.
12 Maua yanatokea juu ya nchi;
majira ya kuimba yamewadia,
sauti za njiwa zinasikika
katika nchi yetu.
13 Mtini unatunga matunda yake ya mwanzoni,
zabibu zinazochanua zaeneza harufu nzuri.
Inuka, njoo mpenzi wangu.
Mrembo wangu, tufuatane."

Mpenzi

14 Hua wangu penye nyufa za majabali,

mafichoni pembezoni mwa mlima,
nioneshe uso wako,
na niisikie sauti yako,
kwa maana sauti yako ni tamu,
na uso wako unapendeza.
15 Tukamatie mbweha,
mbweha wale wadogo
wanaoharibu mashamba ya mizabibu,
mashamba yetu ya mizabibu yaliyochanua.

Mpendwa

16 Mpenzi wangu ni wangu, nami ni wake,
yeye hujilisha kati ya yungiyungi.
17 Hadi jua linapochomoza,
na vivuli vikimbie,
rudi, mpenzi wangu,
na uwe kama paa,
au kama ayala mchanga
juu ya vilima vya Betheri.

3

1 Usiku kucha kwenye kitanda changu
nilimtafuta yule moyo wangu umpendaye;
nilimtafuta, lakini sikumpata.
2 Sasa nitaondoka na kuzunguka mjini,
katika barabara zake na viwanja;
nitamtafuta yule moyo wangu umpendaye.
Kwa hiyo nilimtafuta lakini sikumpata.
3 Walinzi walinikuta
walipokuwa wakizunguka mji.
Nikawauliza, “Je, mmemwona
yule moyo wangu umpendaye?”
4 Kitambo kidogo tu baada ya kuwapita

nilimpata yule moyo wangu umpendaye.
Nilimshika na sikumwachia aende
hadi nilipomleta katika nyumba ya mama yangu,
katika chumba cha yule aliyenichukua mimba.
5 Binti za Yerusalemu, ninawaagiza
kwa paa na kwa ayala wa shambani:
Msichochee wala kuamsha mapenzi
hata yatakapotaka yenyewe.

6 Ni nani huyu anayekuja kutoka jangwani
kama nguzo ya moshi,
anayenukia manemane na uvumba
iliyotengenezwa kwa vikolezo vyote
vya mfanyabiashara?
7 Tazama! Ni gari la Sulemani
likisindikizwa na mashujaa sitini,
walio wakuu sana wa Israeli,
8 wote wamevaa panga,
wote wazoefu katika vita,
kila mmoja na upanga wake pajani,
wamejiandaa kwa ajili ya vitisho vya usiku.
9 Mfalme Sulemani alijitengenezea gari;
alilitengeneza kwa mbao kutoka Lebanoni.
10 Nguzo zake alizitengeneza kwa fedha,
kitako chake kwa dhahabu.
Kiti chake kilipambwa kwa zambarau,
gari lake likanakshiwa njumu kwa upendo
na binti za Yerusalemu.
11 Tokeni nje, ninyi binti za Sayuni,
mkamtazame Mfalme Sulemani akiwa amevaa taji,
taji ambalo mama yake alimvika

siku ya arusi yake,
siku ambayo moyo wake ulishangilia.

4

Mpenzi

1 Tazama jinsi ulivyo mzuri, mpendwa wangu!
Ee, jinsi ulivyo mzuri!
Macho yako nyuma ya shela yako
ni kama ya hua.
Nywele zako ni kama kundi la mbuzi
wakishuka kutoka Mlima Gileadi.
2 Meno yako ni kama kundi la kondoo waliokatwa manyoya sasa hivi,
wanaotoka kuogeshwa.
Kila jino lina pacha lake;
hakuna hata moja lililo pekee.
3 Midomo yako ni kama uzi mwekundu,
kinywa chako kinapendeza.
Mashavu yako nyuma ya shela yako
ni kama vipande viwili vya komamanga.
4 Shingo yako ni kama mnara wa Daudi,
uliojengwa kwa madaha,
juu yake zimetundikwa ngao elfu,
zote ni ngao za mashujaa.
5 Matiti yako mawili ni kama wana-paa wawili,
kama wana-paa mapacha
wajilishao kati ya yungiyungi.
6 Hata kupambazuke na vivuli vikimbie,
nitaenda kwenye mlima wa manemane
na kwenye kilima cha uvumba.
7 Wewe ni mzuri kote, mpendwa wangu,
hakuna hitilafu ndani yako.

8 Nenda nami kutoka Lebanoni, bibi arusi wangu,
nenda nami kutoka Lebanoni.
Shuka kutoka ncha ya Amana,
kutoka juu ya Seniri, kilele cha Hermoni,
kutoka mapango ya simba
na kutoka mlima wapendapo kukaa chui.
9 Umeiba moyo wangu, dada yangu, bibi arusi wangu;
umeiba moyo wangu
kwa mtazamo mmoja wa macho yako,
kwa kito kimoja cha mkufu wako.
10 Tazama jinsi pendo lako linavyofurahisha,
dada yangu, bibi arusi wangu!
Pendo lako linafurahisha aje zaidi ya divai,
na harufu ya marhamu yako zaidi ya manukato yoyote!
11 Midomo yako inadondosha utamu kama sega la asali,
bibi arusi wangu;
maziwa na asali viko chini ya ulimi wako.
Harufu nzuri ya mavazi yako ni kama ile ya Lebanoni.
12 Wewe ni bustani iliyofungwa, dada yangu,
bibi arusi wangu;
wewe ni chanzo cha maji kilichozungushiwa kabisa,
chemchemi yangu peke yangu.
13 Mimea yako ni bustani ya mikomamanga
yenye matunda mazuri sana,
yenye hina na nardo,
14 nardo na zafarani,
mchai na mdalasini,
pamoja na kila aina ya mti wa uvumba,

manemane na udi,
na aina zote za vikolezo bora kuliko vyote.
15 Wewe ni chemchemi ya bustani,
kisima cha maji yanayotiririka,
yakitiririka kutoka Lebanoni.

Mpendwa

16 Amka, upepo wa kaskazini,
na uje, upepo wa kusini!
Vuma juu ya bustani yangu,
ili harufu yake nzuri iweze kuenea mpaka ng'ambo.
Mpenzi wangu na aje bustanini mwake
na kuonja matunda mazuri sana.

5

Mpenzi

1 Nimekuja kwenye bustani yangu, dada yangu,
bibi arusi wangu;
nimekusanya manemane yangu pamoja
na manukato yangu.
Nimekula sega langu la asali na asali yangu;
nimekunywa divai yangu na maziwa yangu.

Rafiki

Kuleni, enyi rafiki, mnywe;
kunyweni ya kutosha, ee wapenzi.

Mpendwa

2 Nililala lakini moyo wangu ulikuwa macho.
Sikiliza! Mpenzi wangu anabisha:
"Nifungulie, dada yangu, mpendwa wangu,
hua wangu, usiye na hitilafu.
Kichwa changu kimeloa umande,
na nywele zangu manyunyu ya usiku."

3 Nimevua joho langu:
je, ni lazima nivae tena?
Nimenawa miguu yangu:
je, ni lazima niichafue tena?
4 Mpenzi wangu aliweka mkono wake kwenye tundu la komeo;
moyo wangu ulianza kugonga kwa ajili yake.
5 Niliinuka kumfungulia mpenzi wangu,
mikono yangu ikidondosha manemane,
vidole vyangu vikitiririka manemane,
penye vipini vya komeo.
6 Nilimfungulia mpenzi wangu,
lakini mpenzi wangu alishaondoka;
alikuwa ameenda zake.
Moyo wangu ulishuka kwa kuondoka kwake.
Nilimtafuta lakini sikumpata.
Nilimwita lakini hakunijibu.
7 Walinzi walinikuta
walipokuwa wakifanya zamu za ulinzi mjini.
Walinipiga, wakanijeruhi,
wakaninyang'anya joho langu,
hao walinzi wa kuta!
8 Enyi binti za Yerusalemu, ninawaagiza:
mkimpata mpenzi wangu,
mtamwambia nini?
Mwambieni ninazimia kwa mapenzi.

Rafiki

9 Je, mpenzi wako ni bora kuliko wengine namna gani,
wewe uliye mzuri kupita wanawake wote?
Je, mpenzi wako ni mzuri kuliko wengine, namna gani,

hata unatuagiza hivyo?

Mpendwa

10 Mpenzi wangu anang'aa, tena ni mwekundu,
wa kuvutia miongoni mwa wanaume kumi elfu.
11 Kichwa chake ni dhahabu safi kuliko zote,
nywele zake ni za mawimbi
na ni nyeusi kama kunguru.
12 Macho yake ni kama ya hua
kandokando ya vijito vya maji,
aliyeogeshwa kwenye maziwa,
yaliyopangwa kama vito vya thamani.
13 Mashavu yake ni kama matuta
ya mimea ya manukato.
Midomo yake ni kama yungiyungi
inayodondosha manemane.
14 Mikono yake ni fimbo za dhahabu
iliyopambwa kwa krisolitho.
Mwili wake ni kama pembe ya ndovu iliyong'arishwa
iliyopambwa na yakuti samawi.
15 Miguu yake ni nguzo za marumaru
zilizosimikwa katika vitako vya dhahabu safi.
Sura yake ni kama Lebanoni,
bora kama miti yake ya mierezi.
16 Kinywa chake chenyewe ni utamu,
kwa ujumla yeye ni wa kupendeza.
Huyu ndiye mpenzi wangu, huyu ndiye rafiki yangu,
ee binti za Yerusalemu.

6

Rafiki

1 Mpenzi wako ameenda wapi,
ewe mzuri kupita wanawake wote?
Mpenzi wako amegeukia njia ipi,
tupate kumtafuta pamoja nawe?

Mpendwa

2 Mpenzi wangu ameenda bustanini mwake,
kwenye vitalu vya vikolezo,
kujilisha bustanini
na kukusanya yungiyungi.
3 Mimi ni wake mpenzi wangu,
na mpenzi wangu ni wangu;
yeye hujilisha kati ya yungiyungi.

Mpenzi

4 Wewe ni mzuri, mpendwa wangu, kama Tirsa,
unapendeza kama Yerusalemu,
umetukuka kama jeshi lenye bendera.
5 Uyageuze macho yako mbali nami;
yananigharikisha.
Nywele zako ni kama kundi la mbuzi
wanaoteremka kutoka Gileadi.
6 Meno yako ni kama kundi la kondoo
wanaotoka kuogeshwa.
Kila mmoja ana pacha lake,
hakuna hata mmoja aliye peke yake.
7 Mashavu yako nyuma ya shela yako
ni kama vipande viwili vya komamanga.
8 Panaweza kuwa na malkia sitini,
masuria themanini,
na mabikira wasiohesabika;
9 lakini hua wangu, mkamilifu wangu,

ni wa namna ya pekee,
binti pekee kwa mama yake,
kipenzi cha yeye aliyemzaa.
Wanawali walimwona na kumwita aliyebarikiwa;
malkia na masuria walimsifu.

Rafiki

10 Ni nani huyu atokeaye kama mapambazuko,
mzuri kama mwezi, mwangavu kama jua,
ametukuka kama nyota zinazofuatana?

Mpenzi

11 Niliteremka kwenye bustani ya miti ya milozi
ili kutazama machipuko ya bondeni,
kuona kama mizabibu imechipua
au kama mikomamanga imechanua maua.
12 Kabla sijang'amua,
shauku yangu iliniweka
katikati ya magari ya vita ya wakuu wangu.

Rafiki

13 Rudi, rudi, ee Mshulami;
rudi, rudi ili tupate kukutazama!

Mpenzi

Kwa nini kumtazama Mshulami,
kama kutazama ngoma ya Mahanaimu*?

7

1 Ee binti ya mwana wa mfalme,
tazama jinsi inavyopendeza miguu yako katika viatu!
Miguu yako yenye madaha ni kama vito vya thamani,

* **6:13** au *majeshi mawili*

kazi ya mikono ya fundi stadi.
2 Kitovu chako ni kama bilauri ya mviringo
ambayo kamwe haikosi divai iliy-ochanganywa.
Kiuno chako ni kichuguu cha ngano
kilichozungukwa kwa yungiyungi.
3 Matiti yako ni kama wana-paa wawili,
mapacha wa paa.
4 Shingo yako ni kama mnara wa pembe ya ndovu.
Macho yako ni vidimbwi vya Heshboni
karibu na lango la Beth-Rabi.
Pua yako ni kama mnara wa Lebanoni
ukitazama kuelekea Dameski.
5 Kichwa chako kinakuvika taji kama Mlima Karmeli.
Nywele zako ni kama zulia la urujuani;
mfalme ametekwa na mashungi yake.
6 Tazama jinsi ulivyo mzuri na unavyopendeza,
ee pendo, kwa uzuri wako!
7 Umbo lako ni kama la mtende,
nayo matiti yako kama vishada vya matunda.
8 Nilisema, “Nitakwea mtende,
nami nitayashika matunda yake.”
Matiti yako na yawe kama vishada vya mzabibu,
harufu nzuri ya pumzi yako kama matofaa,
9 na kinywa chako kama divai
bora kuliko zote.

Mpendwa

Divai na iende moja kwa moja hadi kwa mpenzi wangu,
ikitiririka polepole juu ya midomo na meno.
10 Mimi ni mali ya mpenzi wangu,

nayo shauku yake ni juu yangu.
11 Njoo, mpenzi wangu, twende mashambani,
twende tukalale huko vijijini.
12 Hebu na twende mapema
katika mashamba ya mizabibu
tuone kama mizabibu imechipua,
kama maua yake yamefunguka,
na kama mikomamanga imetoa maua:
huko nitakupa penzi langu.
13 Mitunguja hutoa harufu zake nzuri,
kwenye milango yetu kuna matunda mazuri,
mapya na ya zamani,
ambayo nimekuhifadhia wewe,
mpenzi wangu.

8

1 Laiti ungekuwa kwangu kama ndugu wa kiume,
ambaye aliyanyonya matiti ya mama yangu!
Kisha, kama ningekukuta huko nje,
ningekubusu,
wala hakuna mtu yeyote angenidharau.
2 Ningekuongoza na kukuleta
katika nyumba ya mama yangu,
yeye ambaye amenifundisha.
Ningekupa divai iliyokolezwa unywe,
asali ya maua ya mikomamanga yangu.
3 Mkono wake wa kushoto uko chini ya kichwa changu,
na mkono wake wa kuume unanikumbatia.
4 Binti za Yerusalemu, ninawaagiza:
msichochee wala kuamsha mapenzi
hata yatakapotaka yenyewe.

Rafiki
5 Ni nani huyu anayekuja kutoka nyikani
akimwegemea mpenzi wake?
Mpendwa
Nilikuamsha chini ya mtofaa,
huko mama yako alipotunga mimba yako,
huko yeye alipata uchungu akakuzaa.
6 Nitie kama muhuri moyoni mwako,
kama muhuri kwenye mkono wako;
kwa maana upendo una nguvu kama mauti,
wivu wake ni mkatili kama Kuzimu*.
Unachoma kama mwali wa moto,
kama mwali mkubwa wa moto wa Mwenyezi Mungu hasa.
7 Maji mengi hayawezi kuuzimisha upendo,
mito haiwezi kuugharikisha.
Kama mtu angetoa mali yote ya nyumbani mwake
kwa ajili ya upendo,
angedharauliwa kabisa.
Rafiki
8 Tunaye dada mdogo,
matiti yake hayajakua bado.
Tutafanya nini kwa ajili ya dada yetu
wakati atakapokuja kuposwa?
9 Kama yeye ni ukuta,
tutajenga minara ya fedha juu yake.
Na kama yeye ni mlango,
tutamzungushia mbao za mwerezi.
Mpendwa
10 Mimi ni ukuta,

---

* **8:6** Kuzimu kwa Kiebrania ni *Sheol*, yaani *Shimo lisilo na mwisho.*

nayo matiti yangu ni kama minara.
Ndivyo ambavyo nimekuwa machoni pake
kama yule anayeleta utoshelevu.
11 Sulemani alikuwa na shamba la mizabibu huko Baal-Hamoni;
alikodisha shamba lake la mizabibu kwa wapangaji.
Kila mmoja angeleta kwa ajili ya matunda yake
shekeli elfu moja† za fedha.
12 Lakini shamba langu la mizabibu
ambalo ni langu mwenyewe
ni langu kutoa;
hizo shekeli elfu moja ni kwa ajili yako, ee Sulemani,
na shekeli mia mbili‡ ni kwa ajili
ya wale wanaotunza matunda yake.

Mpenzi

13 Wewe ukaaye bustanini
pamoja na rafiki mliohudhuria,
hebu nisikie sauti yako!

Mpendwa

14 Njoo, mpenzi wangu,
uwe kama paa
au kama ayala mchanga
juu ya milima iliyojaa manukato.

---

† **8:11** Shekeli 1,000 ni kama kilo 11.5. ‡ **8:12** Shekeli 200 ni kama kilo 2.3.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

Creative Commons License

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d